



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI MASASI



(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Kumb. Na. MTC /B.10/3/49

Tarehe: 30/06/2020

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zilizo orozeshwa katika tangazo hili kuomba nafasi zifuatazo:-

**1. KATIBU MUHTASI III NAFASI (01)**

- a. Awe na Elimu ya Kidato cha IV au VI
- b. Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili
- c. Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiingereza na Kiswahili maneno 80 kwa dakika moja.
- d. Awe amehudhuria na kafaulu mafunzo za Computer kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za windows,Microsoft Office,Internet , E Mail na Publisher.

**KAZI NA MAJUKUMU.**

- I. Kuchapa barua na nyaraka mbalimbali.
- II. Kusaidia kutunza kumbukumbu za matukio, miadi , tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- III. Kusaidia kuwapokea wageni na kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikia.
- IV. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada,nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika kazi.
- V. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu husika.
- VI. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**MSHAHARA.**

Ngazi ya mshahara TGS B I

## **2. MTENDAJI WA KIJJI DARAJA LA III NAFASI (01).**

### **2.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Elimu ya kidato cha nne ( Form IV) au sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja ya fani za Utawala ,Sheria Elimu ya Jamii,Usimamizi wa fedha,Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Kijiji Hombolo,Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

### **2.1.2. KAZI NA MAJUKUMU.**

1. Afisa masuhuli na mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji.
2. Kusimamia Ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamzi wa Utawala Bora katika Kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji na kazi katika eneo lake na mkakati wa kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
7. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
8. Kusimamia ,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
9. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalmiko na migogoro ya wananchi.
10. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa kijiji
11. Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

### **MSHAHARA.**

Ngazi ya mshahara **TGS B I**

### **MAELEKEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- a. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45.
- b. Maombi yaambatanishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae) ya muombaji ikionesha wadhamini watatu na taarifa zao sahihi namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kuzaliwa, na picha mbili passport size (ziandikwe majina kwa nyuma)
- c. Testimonial na provisional Statemant of results hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita havitapokelewa.
- d. Waombaji waliostaafu/kustaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- e. Muombaji atakayewasilisha taarifa na sifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa utaratibu.
- f. Barua zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya kiswahili au kiingereza
- g. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.



- h. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate ) kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania
- i. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA level 4 “Basic Technician Certificate” (NTA level 4 ) maombi yao hayatafanyiwa kazi. Kwa sasa Cheti kinachopokelewa ni Technician Certificate” (NTA lever 5) na kuendelea
- j. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili pia kupitia tovuti ya Halmashauri [www.masasitc.go.tz](http://www.masasitc.go.tz)
- k. Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 13/07/2020 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Mji,

S.L.P 447,

**MASASI.**

  
Gimbana Ntavyo  
Mkurugenzi wa Mji  
**MASASI**